OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA NGARA

NGARA HIGH SCHOOL,
S.L.P 60,
NGARA.

April 2022.

SIMU; 0784 616 865/0753 099 624
0756 886 787 MAKAMU MKUU WA SHULE,

Kumb. Na. NGR HIGH .S/S. 5182/2022/3.

MWANAFUNZI: .....

S.L.P: 60

YAH: <u>MAAGIZO MUHIMU YA KUJIUNGA NA NGARA HIGH SCHOOL MWAKA 2022/2023.</u>

1. Ninafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha **V** katika shule hii kwa **mwaka 2022** kwa tahasusi ya **HGL** au **HKL**, shule ya **NGARA HIGH SCHOOL** ni shule ya wavulana tu ipo umbali wa **KM 33** kutoka mji mkuu wa Wilaya ya Ngara na umbali wa **Km 6** kutoka kituo cha Benako na **Km 4** kutoka Kumnazi mpaka shuleni.

2. Shule iko eneo linaloitwa **LUMASI** ni karibu na barabara ya lami kwa wanafunzi wanaotokea maeneo ya Mwanza, Bukoba na Kahama washuke mbele ya beria kuna barabara kushoto iendayo shuleni kuna kibao, cha shule, watakaotokea Karagwe washukie ziro ziro na watembee au wapande pikipiki kabla ya beria kuulia watakiona kibao cha shule ni **KM 1.8** tu kutoka katika kituo hicho. Karibu sana.

3. Muhula wa kuanza, masomo utaanza tarehe **05/09/2022**. hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe **04/09/2022** na masomo yataanza mara tu baada ya shule kufunguliwa. Ni vema kuwasili mapema.

4. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

4.1. SARE YA SHULE.

4.4.1. Sare ya shule hii ni shati jeupe lenye mikono mirefu, Suruali mbili Nyeusi vipimo upana kwa chini **16“ - 18” –** iwe na mfuko mmoja nyuma na turn up chini, modo haziruhusiwi kabisa, viatu vyeusi vya ngozi vyenye kisigino kifupi vya kufunga na kamba na soksi rangi nyeusi .Viatu rangi viwe nyeusi vya kufunga kwa kamba na mkanda wa suluali rangi nyeusi.

- **Kumbuka unapokuja kuripoti uje umevaa sare ya shule.**

4.4.2. Sweta ya rangi ya **Brown (kahawia).** Kumbuka kuja na Jacket Blue/Nyeusi kwa ajili ya usiku prepo (kuvaliwa muda wa kujisomea usiku tu). Sweta ulete mwenyewe. Usipoipata utaikuta shuleni kwa makubaliano yako na muuzaji mwenyewe. ***NB***: ***Maeneo haya yana baridi sana hivyo sweta ni lazima.***

4.2. SARE YA BAADA YA MASOMO (SHAMBA DRESS).

4.2.1. Mwanafunzi anatakiwa kuvaa Suruali ya rangi ya kijani baada ya muda wa masomo . **T – shirt** utaipata shuleni na tai kwa **Tsh. 16,000/=** au pia suluari utashonea shuleni gharama **Tsh. 18,000/=.ili**kuepuka kutofautiana.

4.4.2**.** Sare ya michezo ni tracksuit nyekundu kwa wanafunzi wote na T – shirt ya michezo nyekundu yenye mistari/michirizi mweupe mikononi na bukta yake.

4.4.3.**Nguo za kawaida haziruhusiwi kuonekana shuleni.**

5. ADA NA MICHANGO YA SHULE:-

5.1 Ada ya shule kwa mwaka ni shilingi **70,000/= (elfu sabini).** Unatakiwa kulipa kiasi cha **Tshs. 35,000/= (thelathini na tano elfu)** kwa muhula au zote 70,000**/= (elfu sabini)** kwa wakati mmoja.

5.2 Michango mingine ni kama ifuatavyo;-

5.2.1 20,000/= Ukarabati.

5.2.2 20,000/= Taaluma.

5.2.3 30,000/= Malipo ya wapishi./walinzi

5.2.4 10,000/= Huduma ya kwanza.

5.2.5 6,000/= Kitambulisho na Picha.

5.2.6 2,000/= Nembo ya Shule.

5.2.7 20,000/= Mitihani endelevu na Mock.(joint exam)form v mwishoni.

5.2.8 5,000/= Tahadhali.

5.2.9 5000/= Ghalama ya maji.

ANGALIZO;- Jumla ya Ada na Michango kwa Mwanafunzi ni **Tsh. 188, 000/= (Laki moja na Themanini na nane tu).**

NB. 1) Tsh 10000/=kwa ajiri ya mahafali kuungana na kidato cha sita.

2)Tsh 50400 kwa ajili ya Bima ya taifa ili kutibiwa hospitali yeyote nchini fedha hii ilipwe taslim shuleni.

KUMBUKA; Fedha zote hizi za ada na michango mingine zote ziwekwe kwenye **ACCOUNT** ya shule yenye jina la **NGARA HIGH SCHOOL AC. NO. 32110021916.** Tawi lolote la **NMB,** na mwanafunzi alete risiti iliyotumika kuwekea fedha hizi bank na iwe na jina lake. Mwanafunzi asiyeleta bank pay in slip hatapokelewa. Shule haipokei fedha taslimu. Aida kwa wale wanaolipiwa na wafadhili wakumbuke kuleta uthibitisho wa maandishi yanayoonesha aina ya malipo watakayolipiwa na yatalipwa lini.

6. VIFAA VYA USAFI

6.1 Ndoo Lt 20, na ndoo lita 10 ya kuogea

6.2 Mfagio wa chepeo/au kufagilia nje

6.3 Jembe kwa HKL na panga kwa HGL

6.4 Reubber Squeezer

6.5 Soft broom/ Hard broom

6.6 fyekeo(silesha).

NB. Vyote ni lazima viletwe

7. **VIFAA VYA KULALIA**

7.1. Godoro la $2^1/_2$ x 6

7.2. Shuka 2 za rangi ya BLUU

7.3. Blanket 1, ni lazima kwa sababu eneo hili baridi

7.4. chandarua(net)kuna mbu

8. **VIFAA VYA CHAKULA**

8.1 Sahani

8.2 Bakuli

8.3 Kijiko8.4

8.4 Kikombe cha ½ lita **vifaa vyote viwe vya bati sio plastiki**

9. **VIFAA VYA DARASANI**

9.1. Counter book 7na daftari saba(7)za kufanyia zoezi

9.2 Karamu za Kutosha

9.3 Wanafunzi wa **HKL** na **HGL** waje na Kamusi ya Oxiford Advanced learnes Dictionary kwa kila mmoja.

9.4 Vitabu vya masomo yako kwa tahasusi utakayosoma vinavyostahili au utanunua huku huwa vinaletwa shuleni. Kuanzia **Tsh. 20,000/= @.**

10. Uje na vifaa vyako vya matumizi ya kila siku kama vile taulo, dawa za mswaki, sabuni za kuogea na kufulia, mafuta nk. Ni vyema pia ukaja na sanduku la mbao au la bati kwa ajili ya kutunzia vifaa vyako. Kumbuka nguo za kiraia ambazo si uniform za shule na ambazo hazikutajwa zisiletwe na kuvaliwa shuleni.

11. Uje na rimu 1 ya karatasi **(photocopy paper (A4)** kwa ajili ya majaribio ya mara kwa mara ya mitihani.

12. Uje na picha nne, piga ukiwa umevaa shati la shule na kitambaa cha nyuma **(Background)** iwe ya blue **(PASSPORT SIZE)** (Unaweza piga picha maeneo ya shule kwa gharama mtakayokubaliana na mpiga picha).na uje na picha moja ya mzazi passport size.

13. Uje na nakala ya matokeo ya kidato cha nne **(Result slip).na cheti cha kuzaliwa**

10. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII.

10.1. Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu **Na. 25** ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozi yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya Elimu nchini, unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo;-

10.1.1. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzako na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

10.1.2. Mahudhurio mazuri katika shughuli ndani na nje ya shule.

10.1.3. Kuhudhuria masomo ya jioni **(preparation).**

10.1.4. Kuwahi katika shughuli za shule.

10.1.5. Kuwepo ndani ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule.

10.1.6. Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.

10.1.7. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.

10.1.8. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.

10.1.9. Huruhusiwi Kumiliki simu shuleni.

11.2 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UFUKUZWE SHULE.

11.2.1. Wizi.

11.2.2. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.

11.2.3. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

11.2.4. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.

11.2.5. Uasherati, ushoga, usagaji na Ubakaji.

11.2.6. Kunyoa kwa mtindo usiokubalika.

11.2.7. Kufuga ndevu.

11.2.8. Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kubeli nk.

11.2.9. Kupigana wanafunzi kwa wanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yoyote Yule.

11.2.10. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.

11.2.11. Kudharau bendera ya Taifa.

11.2.12. Kuoa.

11.2.13. Kukataa adhabu kwa makusudi.

11.2.14. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

11.2.15. Kutoroka au kuwa nje ya mipaka ya shule bila idhini ya uongozi.

11.2.16. Kufanya jaribio la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

11.2.17. Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni.

MAMBO MENGINE MUHIMU

12.1. Fomu ya Medical Examination imeambatanishwa ijazwe na mganga mkuu wa Hospitali ya Serikali na ikibidi ikaidhinishwe mara tu unaporipoti shuleni.

12.2. Fomu ya maelezo binafsi ya mwanafunzi mkataba na kutoshiriki katika migomo fujo na makosa ya jinai, fomu hii inakipengele cha mzazi kukiri, kukubaliana na sheria, kanuni na ulipaji wa ada, michango mingine na maelekezo mengine yatokanayo na shule.

12.3 Aje na stemp 4 za kutuma matokeo ya mtihani ya muhula

Tafadhali soma kwa makini maagizo/maelekezo haya na kuyataekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA NGARA HIGH SCHOOL

.....

ABEL J. ELIABU

MKUU WA SHULE

FOMU HII IJAZWE NA IREJESHWE SHULENI

Mimi (Jina la mwanafunzi) ..... Naahidi kuwa mtiifu na kutii sheria na kanuni zote za shule. Sitashiriki katika vitendo viovu kwa muda wote nitakao kuwa shulen.

Mfano: Migomo, fujo,makossa ya jinai nk.

Sahihi ..... (mwanafunzi) Tarehe .....

Mimi (Jina la mzazi) ..... Nakiri kusoma maelekezo yote na masharti ya shule, nakubaliana na sheria, kanuni, kulipa ada, michango na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

Sahihi ..... (Mzazi) Simu ..... Tarehe .....

Namba za simu za watu walio karibu na mwanafunzi

(i) Jina .....No. Simu ..... Uhusiano ..... BABA.

(ii) Jina .....No. Simu ..... Uhusiano ..... MAMA.

(iii) Jina .....No. Simu ..... Uhusiano ..... MEZZI.

.....

ABEL J. ELIABU

MKUU WA SHULE

<u>MEDICAL CERTIFICATE;-</u>

DATE: .....

STUDENT`S NAME: ..... (NAME IN FULL)

THE MEDICAL OFFICER:

.....

.....

.....

I have examine the above named and consider that he/she is physical *fit and mentally*fit/for a full time students. The examination has included the following categories:

(a) Eye – sight .....
(b) Hearing .....
(c) Limbs .....
(d) Venereal diseases .....
(e) Epilepsy .....
(f) Leprosy .....

II. Neuroses .....

III. Other serious Disease .....

Date ..... Signature .....

Station ..... Designation .....